Kweli Tatu za Dhambi na Kweli Tatu za Wokovu

Sura ya 12
Somo la Kusikiza: Uchunguzi wa Agano la Kale Somo la 38

Shabaha: Kujifunza msiba wa dhambi na dawa ya dhambi.

Kama mashariki ilivyo mbali na magharibi, ndivyo alivyoyoweka dhambi zetu mbali nasi. — Zaburi 103:12

Sasa basi, hakuna hukumu ya adhabu juu yao walio katika Kristo Yesu. Kwa sababu sheria ya Roho wa uzima ule ulio katika Kristo Yesu imeniacha huru, mbali na sheria ya dhambi na mauti. — Warumi 8:1, 2

Daudi anatuambia kuwa tunatatua shida yetu ya hatia tunapo kubali kiwango cha Mungu cha kile kilicho sawa na kile kilicho kasoro. Na kiwango hicho kinatushawishi kuwa sisi ni wenye dhambi. Tunapokiri dhambi zetu, Mungu atarejesha nafsi zetu. Hilo ni moja ya matumizi muhimu tunayoweza kutoa kwa hadithi ya dhambi ya Daudi.

Tunaweza jifunza kweli tatu kutokana na dhambi katika maisha ya Daudi. Ya kwanza ni kuwa dhambi zina matukio mabaya. Dhambi kila mara huja na adhabu, yote ya baadaye na ya sasa. Ya pili ni kuwa dhambi ina nguvu nyingi. Ikiwa mtu kama Daudi anaweza letwa chini na nguvu za dhambi, sisi ni nani hata tufikirie kuwa tunaweza kuistahimili? Hatupaswi kuchukulia nguvu za dhambi kuwa ni kidogo. Na ya tatu, dhambi iko na dai la malipo makubwa. *"Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti; bali gharama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu Bwana wetu."* (Warumi 6:23) Huacha alama zake na madoa yake. Na baadhi ya alama hizo na madoa hayo ni yale yasiyotanguka na yasiyo badilika.

Kama pasia jeusi la ukutani mahali ambapo mwuza mawe ya thamani hupanga lulu zake, weusi wa adhabu, nguvu na malipo ya dhambi, hufanya kweli tatu za wokovu kung'ara zaidi. Kwanza Yesu Kristo ameondoa adhabu ya dhambi. Pili, Roho Mtakatifu ni wa nguvu zaidi kuliko nguvu za dhambi na anaweza kuweka nguvu za dhambi mbali na kutawala maisha yetu. Kweli ya tatu ya wokovu ni ya kutatanisha kidogo, kwa vile inahusika na alama na madoa na malipo ya dhambi. Machoni pa Mungu, hata madoa ya dhambi yanaoshwa na msamaha, lakini kwa wakati mwingine alama, na madoa ya dhambi havibadilishwi katika kiwango cha kibinadamu. Matokeo ya dhambi zetu yanaweza kubaki hata kama tumesamehewa kabisa na Mungu.

1. Ukweli au uongo? Biblia inatufunza kutowahi kuwa na hisia za hatia.

2. Ukweli au uongo? Njia mwafaka ya kusuluhisha hisia za hatia ni kutelemsha kiwango chetu na kukana kuwa tulianguka au tulitenda dhambi.

3. Ukweli au uongo? Dhambi ina adhabu.

Ikiwa hujaambiwa lingine la kufanya, basi, chagua jibu moja tu kwa kila swali lifuatalo.

4. Njia ya pekee ya kuondoa adhabu ya baadaye ya dhambi ni?
   a. Kumlipa Mungu kwa ajili ya dhambi zetu
   b. Kwa kusahau dhambi zetu kabisa
   c. Kwa kufanya matendo mengi mazuri
   d. Kwa kukubali kwa imani kazi ya Yesu iliyomalizika msalabani

5. Ni gani kati ya yafuatayo iliyo matokeo ya dhambi kwa wakati uliopo?*(Chagua yote yanayolingana)*
   a. Uhuru
   b. Kuharibu sehemu za maisha yetu
   c. Utumwa kwa dhambi
   d. Ufanisi wa kiroho na kimali
   e. Amani kwa mioyo yetu

6. Tunahitaji kuwa Wakristo kwa muda gani kabla tuweze kushinda dhambi?
   a. Kwa kifupi miaka mitatu
   b. Kwa kawaida baada ya miaka kumi
   c. Kwa ule urefu inayo chukuwa kuwa na imani
   d. Huwa hatushindi kabisa nguvu za dhambi maishani humu. Kila mara huwa na uwezekano wa sisi kutenda dhambi.

7. Kulingana na Biblia, Mshahara wa dhambi ni nini?
   a. Kukariri na kurudia maombi marefu
   b. Dhabihu nyingi za sadaka ya nyama na ya nafaka
   c. Miaka mingi ya majuto
   d. Mauti

8. Nini hufanyikia matokeo na alama za dhambi wakati tumesamehewa?
    a. Mara nyingi matokeo na alama hubaki
    b. Mungu huziondoa kabisa
    c. Tunayasahau ingawa kila mtu mwingine anayakumbuka
    d. Tunayakumbuka lakini kila mtu mwingine anayasahau

9. Mungu alitoa suluhisho ngapi kwa adhabu ijayo ya dhambi?
    a. Moja
    b. Karibu tatu
    c. Nyingi
    d. Hakuna, alishughulikia tu adhabu ya wakati huu.

10. Tunawezaje kuweka nguvu za dhambi chini ya usimamizi?
    a. Hatuwezi
    b. Kwa nidhamu-ya-kibinafsi
    c. Kwa nguvu za Roho Mtakatifu pekee
    d. Kwa kukariri sheria za Mungu

11. Mungu huonaje dhambi zetu baada ya kutusamehe?
    a. Anachagua kutoona dhambi zetu tena
    b. Kila mara yeye huona madoa ya dhambi hizo
    c. Bado humhuzunisha
    d. Hutukumbusha juu ya dhambi zetu kila mara

12. Ni katika njia gani ambazo Mungu hutufanya haki anapotusamehe?
    a. Kwa macho ya wanadamu
    b. Kwa macho yake
    c. Yote
    d. Hakuna

13. Kweli tatu za wokovu ni gani? *(Chagua yote yanayolingana)*
    a. Machoni pa Mungu tunafanywa haki lakini bado tunapitia maumivu ya matokeo ya dhambi.
    b. Roho Mtakatifu anaweza kutupea nguvu za kushinda dhambi.
    c. Kifo cha Yesu msalabani kililipia adhabu ya siku za mbele ya dhambi.
    d. Tunaweza ishi katika dhambi kwa sababu Mungu hutusamehe.

Shetani hataki sisi tujue au tufikirie juu ya kweli hizi tatu za dhambi. Kweli gani za wokovu wa Mungu unazohitaji kuelewa na kupitia zaidi katika maisha yako? Nani unayehitajika kumwambia kuhusu kweli tatu za dhambi na kweli tatu za wokovu?

_____

_____

_____

Mshukuru Mungu kwa msamaha wake, neema na huruma katika maisha yako. Muulize akuwezeshe kuona ushindi zaidi juu ya dhambi katika maisha yako. Muulize Mungu akupe ujasiri wa kushiriki habari njema ya wokovu kwa wengine.

KUZAMA ZAIDI

1. Elezea namna unavyohusiana kwa matumizi ya binafsi na hizi kweli tatu za dhambi. _____
_____
_____
_____

2. Unahusiana vipi kwa matendo ya binafsi, na hizi kweli tatu za wokovu? _____
_____
_____
_____

3. Unahusiana vipi kwa matumizi ya binafsi na zile changamoto zinazohusika na kweli ya tatu ya dhambi na wokovu? _____
_____
_____
_____

4. Husisha maswali haya matatu na majibu yake kwa dhambi ya Daudi. _____
_____
_____
_____

5. Ukweli huu unakwambia nini kuhusu vile Mungu humhifadhi kiongozi aliyeanguka kwenye dhambi? Kuwa Daudi alitenda dhambi katika mwaka wa 16 wa utawala wake na akabaki kuwa mfalme kwa miaka mingine 24 baadaye. Tafakari ukweli kuwa neno la kilatini la *kuhifadhi* linamaanisha, "*kuekeza tena na heshima."* _____
_____
_____
_____

6. Je, mapito haya yote yaliinua au yaliporomosha uwezo wa Daudi wa kuwa mfalme? Vipi?
_____
_____
_____

7. Je, Daudi alikuwa na huruma na kuelewa kwingi au kwa uchache kuwaelekea watu walioanguka dhambini (tafakari Zaburi za Daudi zilizoandikwa wakati huu wa maisha yake na utawala wake kama mfalme)? Fafanua. _____
_____
_____
_____